



Kuona na kusikia

Labda umesiakia kuhusu Derrick Coleman, Derrick mwenye umri wa miaka 23 na anachezea timu ya Seattle Seahawks. Derrick aliweka historia baada ya kuwa kisiwi wa kwanza kujiandikisha kwenye mashindano ya NFL. Hakuzaliwa akiwa na ulemavu huu. Lakini alipokuwa na umri wa miaka mitatu, uwezo wake wa kusikia ulianza kudorola mpaka mwishowe hata sauti ambayo angeweza kuitoa ilikuwa haieleweki na ilikuwa kama kelele tu.

Bila kutisitikika, Derrick alijifundisha kusoma ishara za midomo, na akaendelea kufuatilia mapenzi yake ya kadada. Mpenyo wake mkubwa ulijitokeza wakati timu ya Seattle Seahawks ilimchukua mnamo mwaka wa 2012. Na baada ya miaka miwili, timu yake ikajishidia Super Bowl kwa alama 43 dhidi ya 8. Baada ya kipenga cha mwisho, mashambiki walishangilia kwa mshangilio mkubwa uwanjani, lakini Derrick alikuwa anashikia tu sauti ya makofi kwa mbali mashambiki walipokuwa wakimshangilia alipokuwa akisherehekea pamoja na wachezaji wenzake.

Lakini haikujalisha kwake, kwa kuwa pamoja na kwamba alikuwa hawasikii mashambiki, alijua wanamshangilia na kumsihi aendelee.

Tunaweza kuoanisha maisha ya kikristo tunavyoichukulia sauti ya Mungu na yale maisha ya Derrick. Mara nyingi, huwa tunapata shida kusikiliza sauti ya Roho Mtakatifu inapotuita kutumbu au pia kututia moyo katika nyakati ngumu. Injili ya mtume Yohana inaoanisha maisha yetu na kondoo ambaye ako chini ya mfugaji aliye bora ambaye anajua kuwasiliana na kondoo visiwi! Yesu aliongea kwa sauti ya kusikika, aliwateua wawakilishi wake rasmi, ambao ni mitume, ambao kupitia kwa Roho Mtakatifu, walihubiri, na pia wakaandika waliopaswa kuandikwa kwa niamba ya Kristo.

Lakini Roho wake hatuungeleshi kwa sauti kubwa kama alivyofanya nyakati hizo na mitume. Anaongea nasi moja kwa moja na kwa uhakika kupitia kwa maandiko matakatifu. Zaidi ya hayo, ametuwakilishia mwili wa Kristo, Roho Mtakatifu na pamoja na hayo, walimu stadi ambao kila kizazi wanatusaidia kusikia na kuielewa sauti yake vizuri. La kushangaza tunakumbushwa moja kwa moja vipengele muhimu vya maisha na uwezo wake tunapona vilivyoubwa naye.

“Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. Waebrania 1:1-2)

Kwa hali hii, tunapopata shida kusikia sauti ya Mungu katika maisha yetu, tunatakiwa kujikumbusha kuwa wakati mwingine kuona ni kusikia. Derrick Coleman hakulazimika kuwa anasikia mashambiki wa wa Seahawks ili kujua walikuwa wanamshangilia. Alitakiwa tu kuangalia kutambua walivyomshangilia. Mungu atusaidie kuwa na imani sawia na ile ya Derrick tunapoisikiliza sauti ya yake katika neno lake.

Imeandikwa na: Joseph Tkach, Speaking of LIFE.